Ecolebooks.com

***P320/3***
***FASIHI YA KISWAHILI***
***Paper 3***
***July 2019***
*3 Hours*

# MOCK EXAMINATIONS 2019

***Uganda Advanced Certification of Education***

FASIHI YA KISWAHILI - RIWAYA

**Karatasi ya tatu**

**MUDA: Saa Tatu**

**MAAGIZO:**

i) *Jibu maswali **Matatu tu**.*

ii) *Chagua swali moja kutoka sehemu ya **A, B, CH** au **D.***

iii) ***Sehemu B ni ya lazima kwa wanafunzi wote. Chagua swali moja katika sehemu hii.***

iv) *Usijibu swali zaidi ya moja kutoka kitabu Kimoja wala maswali mawili kutoka kitabu kimoja.*

v) *Nadhifisha mwandiko wako.*

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

## SEHEMU A:

## VIPULI VYA FIGO: Emmanuel Mbogo.

1. a) Dkt. Matoga ni kielelezo mwafaka kwa kizazi kipya. Jadili kwa mujibu wa riwaya nzima. *{Alama 17}*

   b) Tambua dalili zinazodhihirisha uozo au mmomonyoko wa maadili katika jamii Emmanuel Mbogo. *{Alama 16}*

2. a) Dkt. Matoga anafaa kulaumiwa kwa kiwango gani kwa kuchangia changamoto zilizomwathiri maishani? Fafanua kwa kutoa mifano. *{Alama 17}*

   b) Emmanuel Mbogo akipitia wahusika wake amependekeza njia zilizo mwafaka katika kupiga vita dhuluma na uhalifu katika jamii zetu. Taja na uelezee ukirejelea mifano bayana katika riwaya ya Vipuli vya Figo. *{Alama 16}*

### WEMA HAWAJAZALIWA: Ayi Kwei Armah

3. a) Serikali nyingi barani Afrika hupinduliwa madarakani kutokana na changamoto ya ufisadi na hali duni ya maisha. ukirejelea visa na mikasa katika riwaya ya Wema hawajazaliwa, thibitisha ukweli wa kauli hiyo. *{Alama 15}*

   b) Riwaya ya *Wema hawajazaliwa* imebeba ujumbe gani kwa watawala na watawaliwa barani Afrika? *{Alama 18}*

4. a) 'Wema waua' fafanua uyakinifu wa kauli hiyo kwa mujibu wa riwaya ya *Wema hawajazaliwa.* *{Alama 17}*

   b) Ayi Kwei Armah amejaribu kadri ya uwezo wake kuonesha uhalisi wa mfumo wa 'Vuta n'kuvute' katika dunia ya kisasa. Kwa mujibu wa riwaya nzima, toa ukweli wa kauli hiyo ukichambua visa vya migogoro vinavyojitokeza kitabuni. *{Alama 16}*

## *SEHEMU B*

### MISURURU WA USALITI: Mwende Mbatiah.

5. **Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini.**

“Ndama anayeshindwa kunyonya wakati mamake ameshiba atamlaumu nani akikosa maziwa wakati wa kiangazi?” *Ulikuwa usemi maarufu ambao kila mtu aliufahamu.*

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

"Atajilaumu mwenyewe na uzembe wake."

"Umejibu vizuri," *mjomba aliendelea.* "Taifa letu limezaa ndama anayeitwa Wabonde. Nao Wabonde ni nani?"

"Ni sisi mjomba," *Kipanga alijibu.*

"Kwa hivyo ni wakati wetu kunyo. ….."

"Kunyonya," *Kipanga alijazia.*

*Mjomba wake alinusa ugoro, kisha akaendelea*. "Taifa hili ni familia kubwa. Lina makabila chungu nzima. Mengine makubwa, mengina madogo. Mengine tajiri, mengine maskini. Kuna Wapwani, Wanyika, Waziwa, Wamilima na sisi Wabonde. Mungu ametujalia tukawa sisi ndio wenye nyama na kisu. Kila mmoja ametuangalia sisi tumkatie kipande. Hatukatai kuwakatia. Lakini tutakuwa wajinga tukishindwa kujikatia kipande kikubwa na bora zaidi."

"Kweli mjomba," *Kipanga alikubali.*

"Mbunge wetu ni waziri wa serikali. Tena ndiyo macho na maskio ya Mzee. Hana budi kutuletea kipande chetu cha nyama. Miaka yote hii nilikuwa nikimsaidia katika uchaguzi. Tuna uhusiano mzuri. Juzi nimekutana naye nilipokwenda kutafuta daktari wa mifugo. Nikamkumbusha maana ya ujamaa ni kusaidiana. Au vipi mtoto?"

"Ukweli mtupu mjomba."

***Maswali:***

a) Liweke dondoo hilo katika muktadha wake kamili. *{Alama 10}*

b) Toa sababu kuu tatu zilizomchochea mjomba-mtu hadi akajaslia kumpa mpwa wake ujumbe huo maalum uliobadilisha dira ya maisha yake. *{Alama 06}*

c) Dondoo hilo linatilia nguvu maudhui gani kitabuni? Fafanua. *{Alama 06}*

d) Eleza hulka kuu mbili za mjombake Kipanga. *{Alama 04}*

e) Kwa kutoa mifano thabiti taja tamathali za semi tano (5) zilizomo kwenye dondoo hili. *{Alama 08}*

## MWAKILISHI WA WATU: Chinua Achebe

*6.* Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini;

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

"Halo Elsie…………… Unakaribishwa …… Ninafurahi kusikia kuwa uliifurahia. Nimemrudisha nyumbani salama …Ndiyo tu nimerudi…"

*Hasira zake zote alizimaliza kwa kumwita Elsie mbwa jike, na sote tukacheka.*

"Anachotaka kujua ni kama bado uko hapa"

"Unadhani anafahamu?"

"Sidhani na sijali".

*Baadaye, baada ya muda mrefu, tulishuka chini tumeshikana mikono mpaka jikoni, ili Jean akatengeneze kahawa. Sikujali kunywa kahawa wakati huo.*

"Mapenzi yana maana zaidi kwa mwanamke kuliko kwa mwanamume" *akasema akiwa katika hali ya kufikiri, huku akikoroga kahawa yake.*

"Kweli?"

"Kabisa. Kitendo chenyewe hutendeka mwilini mwake. Mwanamume hutumia kitu kilichojitokeza tu kutoka mwilini."

"Kumbe."

***Maswali:***

a) Liweke dondoo hilo katika muktadha wake kamili. *{Alama 12}*

b) Bainisha wazi ni uhusiano wa aina gani uliopo kati ya Mwanamke na mwanamume wanaojibizana katika dondoo hilo. *{Alama 05}*

c) Ukirejelea dondoo, Elsie anayezungumziwa ni mhusika yupi? *{Alama 04}*

d) Mwanamke anadhamiria nini anaposema, *"Mapenzi yana maana zaidi kwa mwanamke kuliko kwa mwanamume"?* Je, unapata taswira gani kutokana na falsafa yake? *{Alama 05}*

e) Huku ukitoa mifano mwafaka, taja na uelezee Fani au mbinu zozote nne (4) zinazojitokeza kwenye dondoo hilo. *{Alama 08}*

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

## SEHEMU CH

## NYOTA YA REHEMA – Mohamed S. Mohamed

**7.** a) 'Ukirejelea mienendo halisi ya wahusika wa kike riwayani, jadili usawiri wa mwanamke katika jamii ya Mohamed S. Mohamed. *{Alama 15}*

b) Jadili umuhimu wa Rehema katika ujenzi wa hadithi ya riwaya ya Nyota ya Rehema. *{Alama 18}*

8. a) Malezi mabaya yanaweza kumwathiri vipi mtoto katika maisha yake? Fafanua kwa kurejelea mifano kitabuni. *{Alama 16}*

b) Said Mohamed ametuwekea ujumbe gani kuhusu malezi mwafaka ya watoto wetu katika jamii zetu za kiafrika? Eleza kwa kutoa mifano kitabuni. *{Alama 17}*

## Dunia yao: *SAID A MOHAMED*

9. a) Jadili uhalisi wa dunia ya mhusika Ndi katika riwaya hii. *{Alama 15}*

b) Kwa mujibu wa riwaya Dunia yao, eleza suala la mmomonyoko wa maadili katika jamii ya kisasa. *{Alama 18}*

10. a) Ukirejelea mifano mwafaka kitabuni, thibitisha ukweli kuwa hadithi ya riwaya ya dunia yao ni ya kisasa. *{Alama 16}*

b) 'Dunia ya kisasa ni dunia inayokosa utaratibu wa dira ya maisha'. Fafanua uyakinifu wa kauli hiyo kwa mujibu wa riwaya ya Dunia yao. *{Alama 17}*

## SEHEMU D

## *NDOTO YA ALMASI – Ken Walibora*

11. a) Suala la elimu limepewaje kipaumbele katika riwaya *Ndoto ya Almasi?* Fafanua. *{Alama 13}*

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

b) Wanafunzi wenyewe wanachangia pakubwa juu ya changamoto zinazokatiza masomo yao. Jadili kwa mujibu wa riwaya ya Ndoto ya Almasi. *{Alama 20}*

12. a) Mwandishi ametuonyesha wazi vikwazo au changamoto gani zinazoifanya jamii yake kubaki nyuma kimaendeleo? Eleza kwa mujibu wa riwaya nzima. *{Alama 18}*

b) Ukijivalisha viatu vya rais wa jamii ya mwandishi, eleza mikakati ambayo ungefanya ili kuikwamua jamii na wananchi wako. *{Alama 15}*

## Nyuso za Mwanamke: Said. A. Mohamed

13. a) Mwanamke ni chanzo cha utengano katika jamii ya Said Mohamed. Thibitisha madai haya kwa mujibu wa hadithi nzima. *{Alama 17}*

b) Jadili nyuso za mwanamke zinazojitokeza katika riwaya ya nyuso za mwanamke. *{Alama 16}*

14. a) Waja wa kizazi cha kisasa hupata maadili gani waisomapo riwaya ya Nyuso za mwanamke? Fafanua. *{Alama 18}*

b) Eleza shida zinazoikumba jamii ya Nyuso za mwanamke. *{Alama 15}*

*****MWISHO*****

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**